

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Simu Na: 026 - 2968433
Nukushi Namba: 026 – 2968832
Tovuti: www.njombetc.go.tz
Barua pepe : td@njombetc.go.tz



S.L.P. 577
NJOMBE.

Unapojibu tafadhali taja,

Kumb.Na: NTC/RM/468/473/1B/21

03 Desemba, 2021

Mkurugenzi,
Vanilla International Co. LTD
S.L.P 32,
NJOMBE.
+255673755755

**Yah: KUSIMAMISHA KUPOKEA WAWEKEZAJI WAPYA NA KUZINGATIA
TARATIBU ZA UWEKEZAJI.**

1. Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu. Pia rejea barua yako isiyokuwa na Kumbukumbu Na. ya tarehe 24/11/2021 iliyopokelewa katika Ofisi hii mnamo tarehe 26 Novemba, 2021 ikiwa na taarifa ya mikataba ya ununuzi wa ardhi na mikataba ya wafanyakazi wa kampuni. Pia rejea barua kutoka Ofisi hii yenye Kumb.Na. NTC/RM/468/473/1B/17 ya tarehe 11 Novemba, 2021 iliyoelekeza Kampuni kuzingatia sheria kanuni na taratibu katika shughuli zako za kilimo cha zao la vanilla.

2. Aidha, katika barua hiyo Ofisi hii ilielekeza kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu kwa kuzingatia yafuatayo :

- Mpango Kabambe (Master Plan) kwa kupata mwongozo wa namna ya kutumia Ardhi ikiwemo kupangwa kimji, kupimwa na kumilikishwa.
- Kupata kibali cha uwekezaji kutoka Mamlaka ya upangaji ambayo ni Halmashauri ya Mji Njombe na Kituo cha Uwekezaji Tanzania.
- Tathmini ya athari ya kimazingira na kijamii ya uwekezaji huo katika eneo hilo.
- Hali ya makazi na mazingira kiafya kwa vibarua na watumishi walioko uwandani/shambani si ya kuridhisha ikiwemo kukosekana kwa vyoo bora, mabafu na mashimo ya taka ukilinganisha na idadi ya watu waliopo na hivyo kusababisha uchafuzi wa mazingira ikiwemo vibarua na watumishi walioko shambani kuoga mtoni.

- Kampuni iliomba leseni ya biashara ya kuuza miche ya zao la Vanilla katika kitalu chake katika Kanisa la Anglikan Mtaa wa Idundilanga na si kilimo cha Vanilla katika Kijiji cha Idunda, hivyo Kampuni inapaswa kupata leseni ya uwekezaji kwa kufata taratibu kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania.
- Mfumo wa ajira kwa vibarua haujazingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na Taratibu za ajira na hivyo hakuna mikataba yoyote kati ya Kampuni na vibarua/watumishi wa waalioko shambani.


3. Ofisi hii inakiri kupokea barua yako isiyo na Kumb.Na ya tarehe 24.11.2021 ikiwa na mada ya kuwasilisha taarifa kuhusiana na kilimo cha zao la Vanilla.Aidha,katika barua yako mambo yafuatayo kwa kuzingatia yaliyopo katika kipengele na. 2 hapo juu yametekelezwa ambayo ni:


- Kuwasilisha mikataba ya ununuzi wa Ardhi wa Ekari 83.75
- Mikataba ya wafanya kazi na
- Taarifa za usajili wa Kampuni BRELLA, OSHA na NSSF.

5. Kupitia barua yako na ukaguzi uliofanyika na Timu ya wataalam kutoka Ofisi hii imebainika kuwa mpaka sasa bado kuna mapungufu mengi hayajatekelezwa ikiwemo; kupanga,kupima na kumilikishwa kwa Ardhi yako,kupata kibali cha uwekezaji kutoka TIC, kurekebisha makazi,vyoo,mabafu na udhibiti wa taka ngumu.

6. Kwa barua hii, Ofisi inakutaka kusitisha mara moja kupokea wawekezaji wapya na kusimamisha uanzishaji wa vitalu vipya vya mashamba mpaka hapo Kampuni itakapozingatia maelekezo ambayo hajazingatiwa katika kipengele Na. 2 hapo juu. Kukiuka maelekezo haya ni kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu za usimamizi na utawala wa Ardhi, usimamizi wa uwekezaji na usimamizi Afya na Mazingira. Hivyo, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Kampuni endapo maelekezo hayo hayatazingatiwa.

Nakutakia utekelezaji Mwema,


K.A. SADICK
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
NJOMBE



Nakala

1. Katibu Tawala wa Mkoa
S.L.P 668
NJOMBE.
2. Katibu Tawala wa Wilaya
S.L.P 1,
NJOMBE.